

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

**MKOA WA MWANZA**

Simu:- 028 – 2530002

FaxNo.:-028 – 2530199

Kumb. Na. MDC/M.10/120/25



Sanduku la Posta 200  
**MAGU.**

24.04.2019

---

**TANGAZO LA AJIRA YA KAZI KWA MKATABA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu kwa kushirikiana na Shirika la AGPAHI anawatangazia nafasi za Ajira kwa Mkataba wa miezi 5 mitano katika fani mbali mbali kwenye vituo vya kutolea tiba Wilayani Magu. Mkataba unaweza kuongezwa kulingana na uwezo wa mhusika.

**1.1: MUUGUZI DARAJA II (NURSE II) - NAFASI 1**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne (F IV) waliofuzu mafunzo ya uuguzi katika chuo kinachotambuliwa na Baraza la wauguzi na wakunga Tanzania au mafunzo ya uuguzi katika ngazi ya cheti na wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

**KAZI NA MAJUKUMU:**

- Kutoa huduma ya ki-uuguzi kwa wagonjwa/wateja kwa kuzingatia sheria, maadili ya taaluma pamoja na miongozo iliyopo katika sehemu za kufanya kazi
- Kutoa elimu ya afya kwa wagonjwa/jamii
- Kufuatilia matatizo ya kiafya ya wagonjwa na jamii katika mazingira yao
- Kutoa huduma za chanjo kwa mama na mtoto na uzazi salama
- Kusimamia, kuratibu na kufuatilia kazi za walio chini yake
- Kufanya kazi nyingine kama atakavyopangiwa na mkuu wake wa kazi
- Anaweza kupangiwa kufanya kazi katika zahanati, kituo cha afya na hospitali ya Wilaya

**Kiwango cha mshahara – Tshs. 600,000= kwa mwezi**

## 1.2: Data Clerk - Nafasi – 3

### Sifa za kuajiriwa

- Stashahada ya Juu au Shahada ya IT, Takwimu au utunzaji wa kumbukumbu kwa njia ya kielektroniki (EMR)
- Awe na uzoefu wa mwaka 1 – 3 katika kazi za Takwimu (Data Management)
- Awe na uzoefu na takwimu za afya (Health Data Experience)
- Awe na uzoefu wa kutumia mifumo ya DHIS2, Ms Excel, Ms Access, EPI – Info, SPSS na uzoefu wa mifumo mingine itakuwa ni sifa ya nyongeza

### Lengo la Ajira:

Ni kuhakikisha Mfumo wa CTC<sub>2</sub> Data Base unafanya kazi kwa usahihi ikiwa ni pamoja na ubora wa Takwimu,

- Utunzaji wa mfumo CTC<sub>2</sub> Data Base
- Kuhuisha CTC<sub>2</sub> Data Base
- Kuingiza takwimu za wagonjwa kila siku na kutengeneza taarifa na kuziwasilisha katika ngazi husika

### Majukumu Makuu:

- Kurudisha faili za wagonjwa ambao hazijajazwa vizuri kwa Mganga (Clinical ili zirekebishwe)
- Kufuatilia takwimu zilizopo kwenye CTC<sub>2</sub> Data Base zilizoingizwa ki-makosa na kuzirekebisha
- Kuhakikisha kila file la mgonjwa linakuwa na fomu za kuchunguza ugonjwa wa kifua kikuu (TB Screening tool) na magonjwa na ngono STI (Screening tool) na kuhakikishwa zinajazwa na Mganga kila mgonjwa anapohudhuria Kliniki
- Kuhakikisha takwimu zilizopo kwenye CTC<sub>2</sub> Data Base kila siku zinaingizwa (Data Cleaning)
- Kutengeneza mpango kazi wa kuboresha takwimu katika kituo husika katika mfumo wa CTC<sub>2</sub> Data Base na katika vyanzo vya Takwimu (Data Source)
- Kuhakikisha matumizi sahihi ya mfumo unafanya kazi kila wakati, kuhuisha antivirus kila siku
- Kuhakikisha unawasiliana na viongozi wako kwa wakati kwa ajili ya ukarabati wa mfumo pindi tatizo linapotokea.
- **Kiwango cha mshahara Tshs. 530,000/= kwa mwezi**



## **MASHARTI YA UJUMLA:**

Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha barua zao kwa Mkurugenzi wakiambatisha nakala ya

- Vyeti vya shule, taaluma na usajili
- Picha mbili ndogo za hivi karibuni
- Wasifu wa mwombaji (CV)
- Mwombaji aandike namba za simu
- Barua zote ziandaliwe kwa mkono.

## **AJIRA**


Mwombaji ataajiriwa kwa mkataba wa miezi mitano (miezi 5) muda ukiisha anaweza kuongezewa muda kulingana na utendaji kazi wake na Shirika la AGPAHI, hadi mradi utakapofika mwisho mwaka 2020.

Maombi yatapokelewa hadi tarehe **09/05/2019** saa **9.30 mchana**, muda wa saa za kazi

Maombi yatumwe kwa,

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Magu,  
S.L.P. 200,  
Magu.**

Imetolewa na



Lutengano G. Mwalwiba,  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
MAGU.**